

Jamii nchini imetakiwa kukataa na kuachana na vitendo vya rushwa ili kupata maendeleo mazuri katika nchi.

hayo yameelezwa na kaimu mkurugenzi elimu kwa umma wa Mamlaka ya kuzuwia rushwa na uhujumu uchumi zanzibar (ZAECA ) Sheha Kombo Hamadi wakati akitoa mafunzo yanayohusu rushwa na uhujumu wa uchumi kwa watu wenye ulemavu, hafla iliyofanyika katika ukumbi wa tume ya uchaguzi huko Maisara mjini Unguja.



Amesema suala la rushwa limekuwa likiwaathiri sana watu waliopo katika makundi maalum na kurejesha nyuma maendeleo yao hivyo ni vyema kukemewa ili jamii iondokane na tatizo hilo.



Aidha ameongezea kwa kusema kuwa serikali imeanzisha Mamlaka ya kuzuia rushwa ambayo ni ZAECA ili watu wapeleke malalamiko yao yanayohusiyana na vitendo vya rushwa hivyo ni vyema kuitumia mamlaka hiyo kwa lengo la kutokomeza vitendo vya rushwa.

Kwa upande wake mmoja ya watu wenye ulemavu kutoka jumuiya ya vijana wenye ulemavu Zanzibar (ZAFEKH) Yumna Mmanga Omar amesema wamekuwa wakikabiliwa na tatizo la rushwa mara kwa mara hivyo elimu waliyoipata itasaidia katika kupambana na vitendo hivyo viovu.



Nae mmoja ya washiriki katika mafunzo hayo Saada Hamad Ali ameiomba Mamlaka ya kuzuia rushwa kuendelea kutoa elimu hiyo kwa familia za watu wenye ulemavu wa akili ili waweze kupambana na rushwa katika jamii zao.

